






Mitandao ya kata itakuwa na mwenyekiti, katibu na mweka hazina na wajumbe watakaounda sekretarieti kutoka kila kijiji. Mitandao ya kata itasaidia kuwa na maamuzi ya pamoja katika usimamizi shirikishi wa misitu.

Kamati za mazingira/ kamati za misitu

Kamati za mazingira hujumuisha wajumbe waliochaguliwa na Mkutano mkuu wa kijiji. Kamati zina wajibu wa kusimamia utekelezaji wa mipango shirikishi jamii katika uhifadhi.

Kikundi cha kuhifadhi misitu ya asili Tanzania (TFCG).

TFCG ni shirika lisilo la kiserikali lenye malengo ya kuhifadhi misitu yenye uwingi wa bioanuwai katika Tanzania.



Mtandao wa Jamii wa Utunzaji Misitu

**Kuzipa uwezo jamii zilizo karibu
na misitu ya asili vijijini kutunza na
kuhifadhi ili wanufaike na
bioanuwai za misitu.**

Wasiliana:

Mtandao wa Jamii wa Utunzaji Misitu
Jengo la tume ya sayansi na teknolojia, Gorofa ya pili,
Chumba namba C24-25 na C34-35
Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,
P.O. Box 23410, Dar es Salaam, Tanzania
Tel/Fax: 022-277 59 92,
E-mail: tfcg@twiga.com



Tanzania Forest Conservation Group (TFCG)
Kikundi cha kuhifadhi Misitu ya asili Tanzania



Tanzania Forest
Conservation Group (TFCG)
Kikundi cha kuhifadhi Misitu
ya asili Tanzania



Ustawi na kuimarika kwa misitu ya asili Tanzania kunategemea ushirikiano miongoni mwa washikadau katika sekta ya uhifadhi wa misitu ya asili. Mtandao wa Jamii wa Utunzaji Misitu unaziunganisha jamii zinazoishi kando kando ya misitu ya asili vijijini zinazoshiriki katika usimamizi shirikishi jamii wa misitu ya asili.

Misitu ya asili Tanzania.

Misitu ya asili ya ukanda wa pwani na safu za milima ya mashariki ni hazina kwa Taifa na dunia kwa ujumla. Misitu hii ni vyanzo vya maji ambayo hutumiwa na mitambo ya kuzalisha umeme na hutoa maji kwa matumizi ya watu katika mikoa ya Iringa, Morogoro, Tanga na Dar es Salaam.

Dira ya mtandao:

Ni kuziwezesha jamii zinazoishi karibu na misitu ya asili vijijini kuwa na uwezo wa kutunza na kuhifadhi misitu ya asili Tanzania.

Malengo ya mtandao:

Malengo makuu ya mtandao ni haya yafuatayo.

- Kuimarisha mawasiliano miongoni mwa washikadau katika sekta ya misitu kwa lengo la kubadilishana uzoefu juu ya ushirikishwaji wa Jamii wa utunzaji hifadhi za



- Kuziwezesha kamati za mazingira na mitandao katika ngazi ya vijiji, kata na tarafa kushiriki kikamilifu katika kusimamia misitu yao kwa kutoa mafunzo na ushauri wa kitaalamu.
- Kuziunganisha jamii zinazoishi kandokando ya misitu ya asili ili kuwa na sauti ya pamoja katika usimamizi shirikishi jamii wa misitu.
- Kuwezesha upatikanaji wa habari kutoka kwa washikadau wanaojihusisha na uhifadhi wa misitu asili.

Muundo wa mtandao

Wanachama:

Kuna aina mbili za wanachama.

- Mitandao ya wanamazingira ya kata au tarafa ya vijiji vilivyo kando kando ya misitu ya asili.
- Taasisi za kiserikali na mashirika yasiyo ya kiserikali yanayo jishughulisha na uwezesaji wa jamii katika uhifadhi wa misitu.

Ada ya uanachama.

Wanachama wa Mtandao watalipa ada ya uanachama kama itakavyo pangwa na mkutano mkuu wa mwaka.



Kazi za Mtandao

- Kuziwezesha jamii kujifunza pamoja katika usimamizi shirikishi jamii kwa njia za mikutano na ziara za mafunzo miongoni mwa washikadau.
- Kuchapisha jarida la kiswahili na majala da ya mafunzo, ili kupashana habari za ushirikishwaji wa wananchi katika uhifadhi wa misitu ya asili.
- Kuratibu kongamano la wanamtandao wa Jamii wa Utunzaji Misitu ya litakalo fanyika mara moja kwa mwaka.
- Kuratibu ziara za mafunzo kwa kamati /mitandao ya wanamazingira. Mafunzo kwa kupashana habari na kubadilishana uzoefu.



Katika ngazi ya Kitaifa kazi za Mtandao zinaratibiwa na kitengo cha Mtandao wa Jamii wa Utunzaji Misitu kilichopo TFCG Dar es Salaam. Majukumu ya kitengo ni kuhamasisha jamii kushiriki kwenye shughuli za mtandao na kusaidia katika utafutaji wa fedha.

Kamati ya mtandao:

Mtandao unasimamiwa na kamati ya mtandao inayochaguliwa na mkutano mkuu wa mwaka. Wajumbe wa kamati ya mtandao huchaguliwa kutoka miongoni mwa washikadau wa sekta ya uhifadhi misitu.

Mitandao ya kata au Tarafa.

Kamati na vikundi vya wanamazingira za vijiji vilivyo kando kando ya misitu wa asili wanaweza kuunda Mtandao mdogo katika kata au tarafa.